# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL9

# KISWAHILI PAPER 3 ANSWERS

## 1.SEHEMU A: (Alama 20 )

### USHAIRI

1. a) Tarbia –mishororo mine katika kila ubeti.

Mathnawi – vipande viwili ukwapi na utao)

katika kila mshororo.
Mtiririko –vina vya ndani na vya nje,vina urari keketo. (Hoja zozote 2x1=2)

b) Kuboronga/kubananga/kufinyanga sarufi –fumbo moja kufumbua badala ya kufumbua fumbo moja dhima ni kutosheleza urari wa vina.

Mazida –Molia badala ya Mola –dhima ni kutosheleza idadi ya mizani.
Pia kuna Injilia badala
Ya injili.

Dhima –kutosheleza mizani. (Hoja zozote 2x2=4:

Tarbini :Kutambua idhini pekee-0

Dini inatumiwa kama unyenzo ya kuijiendeleza kiuchumi. (Hoja 1x2=2)

Toni ya kuonya/kutahahadharisha- anamwonya
e) Nasahau –Twayatia akilini.

Utohozi

-Rupia –rupee.

Tashbihi/mshabaha/ufananisho –mbegu tele zipandeni,ja magari na rupia. (Hoja zozote 2x1=2 )

mfano na asili ya neno hilo.
f) Ulimwengu/jamii ingawa na unafiki wa ni jukumu letu kuukomesha. (Hoja 1x1=1)
g) Umuhimu wa kutoa sadaka husisistizwa katika runinga na radio/vyombo vya habari.

Mchungaji/Ovasia anafanya mambo yapi ya kisiri/pembeni /mafichoni. (Hoja 4x1=4
Lazima mtahiniwa afungu aya ndipo atumizwe.)

h) Ukabatizwa ili utakasike/uwe safi/uwe mwokovu kamili.(Hoja 1x1=1)

## 2. SEHEMU B: (Alama 20 )

### TAMTHILIA

2. a)

- Msemaji ni Diwani III.
- Anawaambia Meya ,Diwani I na Diwani II.
- Mahali ni katika ofisi ya Meya.
- Wamefaika kwa mwaliko wa Meya.
- Wanajadili suala la wafanyakazi kutoridhika na namna ya kukabiliana nalo. (Hoja zozote 4x1=4)

- .Lazima hoja za kwanza tatu zijitokeze kasha mojawapo ya mbili za mwisho)
- Mishahara duni ya wafanyakazi wa Baraza la Cheneo.
- Huduma hafifu za kiafya.
- Uimla katika utawala wa cheneo- wafanyakazi wanapuuzwa.
- Ubaguzi wa watawala wa Cheneo (utabaka) viongozi ndio wanaopendelewa.
- Elimu duni kwa watoto wa wafanyakazi.
- Kucheleweshwa kwa mishahara ya wafanyakazi.
- Njaa iliyothiri hata kusababisha utapia mlo kwa watoto mf.Dadavuo Kaole.
- Usaliti wa viongozi-wanajihudumia badala ya kuwahudumia raia waliowachagua.
- Matumizi ya nguvu zilizokithiri kuzima maandamano ya wafanyakazi m.f askari kutumia bunduki na virungu. (Hoja zozote 5x2=10)

c)

- Matumizi ya nguvu kukomesha migomo m.f:kutumia silaha
- Uenezaji wa uzushi/propaganda m.f madai kwamba Cheneo ni mji wenye mafanikio na sera nzuri za utawala
- Matumizi ya vitisho mf:wafanyakazi wafutwe kazi na vijana waajiriwe.
- Matumizi ya hila/uwingo mf:madai kwamba dawa zilikuwa mjiani.
- Uendelezaji wa ubaraka/ukaragosi (Bili,Diwani I,Diwani II).
- Mbini ya tenga –tawala –vibaraka kupendelewa na wafanyakazi kubaguliwa. (Hoja zozote 4x1=4)

d) Msemo –kuwaka moto wa mafanikio.

Nidaa –kumbuka kila kilio kina maana yake! (Hoja zozote 2x1=2)

3.
- Unyakuzi wa rasimali m.f:Meya na wafuasi wake kunyakua vipande vya ardhi.
- Wizi na uuzaji wa vifaa vya umma kwa manufaa ya kibinafsi. M.f Meya na vibaraka wake kupanga nyama ya kuuza fimbo ya Meya.
- Matumizi mabaya ya mamlaka/vyeo.
- Kujifaidi –Meya kutumia cheo chake kuwatisha wapinzani wake.
- Huduma hafifu za kimsingi ilhali kodi iliotozwa m.f Hospitali na zahanati kukosa dawa,ukosefu wa majisafi lich ya kodi waliyotozwa.
- Ajira kutolewa kidugu au kwa kufahamiana –mhazili aliajirishwa ma Meya.
- Ubadhinifu/ufiyayi wa fedha za umma-Meya na vibarak wake kustarehe katika mkahawa wa kajifahari,kulipwa kwa bili wa mhubiri wasio waajiriwa.
- Njama ya kupinda au kukiuka haki/sheria-Pendekezo la Bili na mpango wa Meya kutumia mahakama kujifaidi.
- Utafutaji wa raia wa kigeni kwa hila –Meya kutaka mwanawe atakayezaliwa apate uraia wa kigeni/ugenini.Bili pia anatamani hivyo.
- Matumizi ya vishawishi kutafuta uungwaji-Meya kuwapendelea madiwani katika nyongeza ya mishahara na marupurupu.
- Kubuniwa kwa vyeo ghushi/bandia-Bili na mhubiri kupewa vyeo vya washauri wa Meya ili walipwe.
- Rasmali za nchi/mji kutumiwa kwa maslahi ya kibinafsi-Meya kuelimisha wanawe ng'ambo na mkewe kujifungilia kule kwa gharama ya fedha za umma. (Hoja zozote 10x2=10)

## 3. SEHEMU C: (Alama 20 )

**RIWAYA**

4. a)

- **Mnenaji ni Amani.**
- **Anamwambia Mtemi Nasaba Bora. (Hoja 2x1=2)**

**b)**

- **Balagha /mubalgha –kama huyu mwanangu basi mlizaa na nani?**
- **Methali –Pasi ya viganja viwili kofi hazilii. (Hoja 2x2=4: Lazima mtahiniwa athibitishe ndipo atuzwe alama 2 kwa kila hoja.mfano pekee wa tamathali:-alama 1)**

- **C) Msemewa ni Mtemi Nasaba Bora.**
- **Kupenda ufahari au utukufu –alienzi kutambulika kuwa jabari au kiongozi wa pekee.**
- **Ukatili wake –anampuuza mbwa wake badala ya kumshughulikia kiafya;amri Amani wa Imani watume mbaroni wa kuzuiliwa :manaji n.k.**
- **Uendezaji wa kisasa-chuki yake dhidi ya nduguye mwalimu Majisifu.**
- **Ufuska /usherati-anajhusisha kimapenzi na Lowela hata mwanaharamu uhuru.**
- **Ufisadi –ananyakuwa afrdhi ya watu,namna aliyopata cheo cha utemi,kimapendeleo n.k.**
- **Mapuuza –uchafu katika mazingira yake,kuugua kwa Amani,vilio vya raia kupuuzwa.**
- **Uimla/udikteta –alifanya maamuzi yake bila kuwashiririkisha wanajamii.**
- **Matumizi mabaya ya cheo au mamlaka-anatumia utemi wake kuwadhulumu wanajamii mf:Amani kusingiziwa kwa babake motto uhuru.**
- **Wivu –anavyompiga Amani na kumtimua mkewe kwa kuwatuhumu kuwa wapenzi –eti aliwafumania.**

- **Utepetevu –hatekelezi majukumu ya nyumba au ndoa –mkewe Zuhura ni mpweke.**
- **Uhalifu –wizi wa ardhi n.k. (Hoja zozote 7x2=14)**

**5.**
- **Kielezo bora cha uzalendo –wanafaa kuonyesha upendo kwa jamii kwa kujitoa mhanga kusaka haki mf:Amani na Imani Madhubuti.**
- **Uendelezaji wa harakati za ukombozi –kutoa mwelekeo wa kuzingatiwa katika kuikomboa jamii.Amani na Imani wanaongoza wanasokomoko kufanikisha ukombozi wa kisiasa,kijamii na kiuchumi.**
- **Kuwazindua wanajamii-Amani na Imani wanabainisha maovu ya utawala wa Mtemi Nasaba Bora na mwalimu Majisifu hata kukawa na haya ya mapinduzi.**
- **Kuendeleza vipawa –Amani anaendeleza kipawa cha utunzi/uandishi (mswada wake wa riwaya Kidagaa Kimemwozea.**
- **Kujitegemea katika maisha –vijana wa Sokomoko hata wageni wanatafuta ajira ili kujiruzuku mf:Amani ,Imani ,D.J n.k.**
- **Kubadili mitazamo hasi na finyu-Imani anabadili mtazamo wa wanajamii kwa kukiuka mwiko au marufuku ya kunywa maji yam to Kiberenge;mtazamo kuhusu watoto wenye kasoro n.k.**
- **Kudumisha maadili ya jamii/heshima-Amani na Imani wanakaa pamoja bila kuvunjiana heshima.**
- **Kuwajali na kuwahurumia wengine-Amani anakubali kukilea kitoto Uhuru,Imani anawatunza watoto wa mwalimu Majisifu licha ya ulemavu wao.**
- **Kielezo cha ukakamavu-Amani na Imani wanajitosa katika uwanja wa ukombozi wenye changamoto nyingi;wanavyokabiliwa na waovu kama Mtemi Nasaba Bora.**
- **Kielezo cha maridhiano/msamaha- Amani anamsamehe Mtemi Nasaba Bora kwa maovu aliyomtendea.**
- **Kuwa na maono- DJ anatabiri kupanda vyeo kwa Amani na Imani na wanatokea kuwa ….**
- **Kuendeleza utangamano wa wanajamii-Amani na Imani wanvyoshirikiana licha ya asili na malengo tofauti;Amani na madhubuti kuwa uhuru katika elimu/kupevuka kiakademiaAmani,Madhubuti n.k (Hoja zozote 10x2=20)**

## 4.SEHEMU D: (Alama 20 )

### HADITHI FUPI

**6.**
- **Tendo la kijana mvulana msafiri kumwachia Esther kuti garini si kawaida kuchungana na mila na desturi za kiafrika.**
- **Hali ya anga kumpumbaza Esther hata akazidisha starehe za usingizi.**
- **Esther kutobadilishiwa zamu kuwa ya mchana badala ya kuahudiwa na Grace anataharuki.**
- **Msafiri mmoja ana shaka ikiwa gari la abirioa liliruhusiwa kuingia eneo la uwanja wa ndege.**
- **Esther ana shaka ikiwa ataweza kufanya kazi huku akisomea usekritari.Anahofia kushindwa.**
- **Esther anatilia shaka usalama katika vilabu vya Nairobi amabamo Kamata alitaka kumpeleka.**
- **Esther ana shaka iwapo Kamata alifika kazini.Alihitaji kupitiwa naye ilivyokuwa desturi lakini sasa ana shake.**
- **Esther ana shaka ikiwa Kamata bado alimpenda/alijali Grace.**
- **Esther anatilia shaka uhusiano wake na Kamata kwamba hakupokea na kuitikia simu zake.**
- **Mtega katika uwanja ana shake ya kuachwa na ndege.**
- **Esther ana shaka ikiwa Kamata angempta mzungu amkabidhi pesa zake.**
- **Mzungu msafiri ana shaka kwa sababu ya kuihirishwa mara mbili kwa kuondoka kwa ndege.Alihofia kuchelewa kuhudhuria mkutano muhimu Dubai.(Hoja zozote 10x2=20**

**7. a)**

- Hii ni kauli ya mwandishi.
- Anamrejelea Kananda.
- Mahali ni nyumbani kwao Kananda.
- Kananda alikuwa amewaomba wazazi wake na ami yake darubini. (Hoja 4x1=4

**b)**

- Inabidi Kananda aache shule ili anasaidia wazazi kupata riziki.
- Ajira ya mapema kwa Bwana Mwatela ili kupata rizik
- Kananda anabidiwa kumtisha Bwana Mwatela kuwa angeacha kazi.Hili ni kutaka kuendeleza ukware kwake.
- Kananda kustahimili uovu wa kunyemelewa wa Bwana Mwatela.Alihofia kuachishwa kazi na siri ya uovu huo kufichuliwa
- Kananda anatenda kazi yake ya ulezi kwa Weledi hata mama Sami anaahidi kumfaa wakati angejifungua.
- Aliporudishwa Kenya kutoka Kongo,alifanya juhudi kuwatafuta Bwana na Bibi Mwatela ili amwone mwanawe.Alienda Nairobi na ami yake kuwatafuta.
- Kananda kuvumilia kubeba mimba hadi akamza mwanawe Mwakitawa badala ya kuavya mimba.
- Juhudi za Kananda kutaka kumwona mwanawe Mwakitawa nyumbani kwa Mwatela.Anastahimili hali mbaya ya anga (baridi) usiku kucha
- Kananda anafanya juhudi za ufaraguzi wa kutaka kutumia darubini kumtazama mwanawe.Anafanikiwa kupata darubini kupitia mwanawe Mbao.
- Anatumia darubini kumtamaza mwanawe Mwatitawa mara kadha hadi alipogunduliwa.
- Kananda anakubali fidia ya Bwana Mwatela.Anakuwa tajiri asiyetarajiwa kwa kumiliki nyumba ya kifahari aliyopewa na Bwana Mwatela.

## 5.SEHEMU E: (Alama 20 )

### FASIHI SIMULIZI

8. **a)**

- Ina gharama ya chini zaidi katika ukusanyaji wa data.
- Mtafiti anaweza kufikia idadi kubwa ya watu kwa kipindi kifupi.
- Inaweza kutumiwa katika mahijiano kama mwongozo kufidia udhaifu wa mhojiwa.
- Humpa mhojiwa muda wa kuwazia maswali na kufanyia uchunguzi kabla ya kuyajibu.
- Hojaji aghalabu hazina athari ya mtafiti kwa kuwa hujazwa kama hayupo.Habari za kweli hujazwa.
- Hija inaweza kudalishwa kulingana na kiwangao cha wajazaji au wahojiwa. (Hoja zozote 4x1=4)

**b)**

- Gharama ya utafiti inaweza kuwa kubwa kiwango cha kutomudiwa na mtafiti.
- Mtazamo hasi wa wanajamii kuhusu hoja huenda ukwafanya wasijaze.
- Baadhi ya wanajamii wanaweza kumshuku mtafiti kuwa mpelelezi na wakakataa kutoa habari.
- Utafiti unaweza kukwamizwa kwa baadhi ya wahojiwa kudai malipo kabla ya kuhojiwa.
- Mbinu nyingine kama vile hojaji hujitaji wanaojua kusoma na kuandika.Wasiojua

**watakwamiza au wapotoshe matokeo.**

- **Vizingiti vya dini-Imani kwamba matendo ya fasihi simulizi ni ya kinyume cha imani yao.**
- **Kupotea au kufisidiwa kwa vifaa vya kuhifadhi data.**
- **Uchache wa wazee au wataalamu wa fasihi simulizi.**
- **Vikwazo vya watawala-huenda wakakataa kutoa idhini ya kufanya utafiti.**
- **Wadhamini ndo mara nyingi huamua mambo yanayochunguzwa,mahali pa kuchunguza na mawanda au upeo wa kuchunguza kwenyewe.**
- **Mtafiti huenda asiwe na wakati wa kutosha kuwahoji watu wengi.**
- **Matatizo ya uchukuzi na mawasiliano.**
- **Matatizo ya kibinafsi mf:mhoji kugeuka,mhojiwa,kutojua lugha ya wahojiwa n.k**
- **Ukosefu wa usalama.**
- **Tatizo kutafsiri data kutoka lugha za kijamii.(Hoja 8x2=16)**